

# UQAB
Jarida la

Toleo 30 - Shawwal 1440 H / Julai 2019 Miladi

**Vipi Khilafah Itakavyo Hifadhi Haki za Kisiasa za Wanawake**

**Vipi Khilafah Itakavyo Wadhamini Wanawake Haki Zao za Kielimu**

**Vipi Khilafah Itakavyo Unda Nidhamu ya Elimu ya Daraja ya Juu Kabisa**

**Vipi Khilafah Itakavyo Kuwa Dola Inayo Ongoza Katika Sayansi na Teknolojia**

**Vipi Khilafah Itakavyo Unda Familia Imara**



## Vipi Khilafah Itakavyo Linda Heshima ya Wanawake

# Vipi Khilafah Itakavyo Linda Heshima ya Wanawake

Uislamu umeipa hadhi kuu heshima kwa wanawake. Dalili kadha wa kadha za Kiislamu zinawawajibisha wanaume na mujtama kuwatazama na kuamiliana na wanawake kwa heshima na daima kulinda hadhi yao.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ لاَ يَحِلُّ لَكُمْ أَن تَرِثُواْ النِّسَاء كَرْهًا وَلاَ تَعْضُلُوهُنَّ لِتَذْهَبُواْ بِبَعْضِ مَا آتَيْتُمُوهُنَّ إِلاَّ أَن يَأْتِينَ بِفَاحِشَةٍ مُّبَيِّنَةٍ وَعَاشِرُوهُنَّ بِالْمَعْرُوفِ فَإِن كَرِهْتُمُوهُنَّ فَعَسَى أَن تَكْرَهُواْ شَيْئًا وَيَجْعَلَ اللّهُ فِيهِ خَيْرًا كَثِيرًا

"Enyi mlio amini! Si halali kwenu kuwarithi wanawake kwa nguvu. Wala msiwadhikishe ili mwapokonye baadhi ya mlivyo wapa isipokuwa wakifanya uchafu ulio wazi. Na kaeni nao kwa wema, na ikiwa mmewachukia, basi huenda mkakichukia kitu, na Mwenyezi Mungu ametia kheri nyingi ndani yake." [An-Nisa: 19]

Mtume (saw) amesema: «إِنَّمَا النِّسَاءُ شَقَائِقُ الرِّجَالِ، مَا أَكْرَمَهُنَّ إِلَّا كَرِيمٌ وَمَا أَهَانَهُنَّ إِلَّا لَئِيمٌ» "Hakika wanawake ni ndugu wa baba na mama kwa wanaume. Hakuna awakirimuye isipokuwa mkarimu na hakuna awafedheheshaye isipokuwa muovu." [Abu Dawood]

Mtume (saw) amesema: «اسْتَوْصُوا بِالنِّسَاءِ خَيْرًا» "Watendeeni wema wanawake." [Bukhari na Muslim]

• Hivyo basi, Khilafah itaweka hifadhi ya hadhi na usalama wa wanawake kama nguzo kuu ya sera ya dola. "Mwanamke ni heshima ('ird) ambayo ni lazima ihifadhiwe." (Kifungu cha 112, Kielelezo cha Katiba ya Al-Khilafah cha Hizb ut Tahrir)

• Dola itahamasisha uchamungu (Taqwa) ndani ya mujtama unaokuza aqliya ya kujihisabu na uwajibikaji katika namna wanaume wanavyo watazama na kuamiliana na wanawake.

[يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَلْتَنظُرْ نَفْسٌ مَّا قَدَّمَتْ لِغَدٍ وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ] "Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na kila nafsi iangalie inayo yatanguliza kwa ajili ya Kesho. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu anazo khabari ya mnayo yatenda." [Al-Hashr: 18]

• Khilafah itatumia nidhamu zake za kisiasa, kielimu na vyombo vya habari pamoja na njia nyinginezo zilizo mikononi mwake ili kuimarisha mtazamo wa heshima kwa wanawake.

• Uislamu umeharamisha ghasia za aina yoyote dhidi ya wanawake – iwe nyumbani au barabarani. Mtume (saw) amesema: «لاَ تَضْرِبُوا إِمَاءَ اللَّهِ» "Msiwapige watumwa wa kike wa Mwenyezi Mungu." [Ibn Majah]

• Kuupa sura ya ngono mujtama pamoja na aina zote za kuwafanya kuwa vyombo, kuwanyanyasa na kuwadunisha wanawake zitaharamishwa chini ya Khilafah. Dola pia inawaharamisha wanawake kujiingiza katika kazi au huduma yoyote inayoutumia urembo au mwili wake na kumshusha hadhi yake.«وَنَهَانَا عَنْ كَسْبِ الأَمَةِ إِلاَّ مَا عَمِلَتْ بِيَدِهَا وَقَالَ هَكَذَا بِأَصَابِعِهِ نَحْوَ الْخَبْزِ وَالْغَزْلِ وَالنَّفْشِ» Rafi bin Rifaa (ra) asimulia, "(Mtume (saw) ametukataza juu ya chumo kutokana na mtumwa wa kike isipokuwa kwa yale aliyo yachuma kwa mkono wake na akasema 'hivi' kwa kuashiria kwa vidole vyake, mithili ya kuoka mkate, kushona, na kuchonga." [Abu Dawud]

"Wanaume na wanawake hawapaswi kufanya kazi yoyote inayo hatarisha maadili au kusababisha ufisadi katika mujtama." (Kifungu cha 119, Kielelezo cha Katiba ya Al-Khilafah cha Hizb ut Tahrir)

• Nidhamu kamilifu ya kijamii ya Kiislamu imeorodhesha hifadhi ya hadhi ya wanawake kuwa kitovu cha sheria zake na inacheza dori kuu katika kusimamisha heshima kwa wanawake kama msingi mkuu wa mujtama. Sheria hizi za kijamii za Kiislamu hudhibiti maingiliano kati ya wanaume na wanawake, ikiyaelekeza mahusiano ya kijinsia katika ndoa pekee.

"Utenganishaji baina ya jinsia ni wajib, hawapaswi kukutana isipokuwa kwa hitajio ambalo sheria inaliruhusu au kwa lengo ambalo sheria inawaruhusu wanaume na wanawake kukutana kwalo, kama vile biashara au Hajj." (Kifungu cha 113, Kielelezo cha Katiba ya Al-Khilafah)

"Wanawake wameharamishwa kuwa faragha (khulwah) na wanaume wowote ambao si mahram zao, vile vile wameharamishwa kuonyesha mapambo yao au kufichua miili yao mbele ya wanaume wa kando." (Kifungu cha 118, Kielelezo cha Katiba ya Al-Khilafah cha Hizb ut Tahrir)

• Nidhamu ya kijamii ya Kiislamu inatoa muundo ambao kwao hulinda kivitendo hadhi ya wanawake: Kwanza, kupitia kutekeleza upya msingi kuwa wanawake sio vyombo vya kuanikwa hadharani ili wanaume kujistarehesha, bali pia kuhifadhi mahusiano safi kati ya jinsia mbili yanayo hakikisha maingiliano yao hayarahisishwi au kuzuiwa kupitia ubabaishaji wa kingono. Hili huasisi ushirikiano wenye matunda, na manufaa kati ya wanaume na wanawake katika nyanja zote za maisha. Na pili, kupitia kuunda mazingira safi na ya kujiepusha na ufuska ambayo matamanio ya kingono hushibishwa kwa namna inayoleta wema katika mujtama badala ya madhara. Yote haya husaidia kudumisha mazingira ya heshima adhimu kwa wanawake, yakipunguza ghasia na uhalifu mwengineo dhidi yao. Natija yake itakuwa kuunda mujtama chini ya Khilafah ambao wanawake wataweza kusoma, kufanya kazi, na kusafiri katika mazingira salama.

• Kupitia nidhamu yake ya kielimu na kimahakama,

***Endelea Uk..3***

Khilafah itafanya bidii kuondoa taasubi za kimila zinazowadunisha wanawake au kuwapokonya haki zao za Kiislamu, pamoja na kuondoa tabia dhalimu za kitamaduni kama vile ndoa za lazima na mauwaji ya heshima. Pia itaharamisha kuingia kwa fikra, picha, vitabu, majarida, au mziki wowote ndani ya mujtama wake yanayo dunisha hadhi ya wanawake.

• Khilafah itatabikisha adhabu kali za Uislamu kwa aina yoyote ya unyanyasaji dhidi ya wanawake ikiwemo ghasia na ubakaji. Kanuni hizi dhidi ya uhalifu ikiwemo upigaji bakora kwa ajili ya uzushi au upigaji mawe hadi kifo kwa ajili ya uhalifu mwengineo dhidi ya hadhi yao. Dola inawajibishwa kuwa na nidhamu barabara ya kimahakama ili kukabiliana haraka na uhalifu kiasi ya kuwa wanawake wataweza kutafuta haki mara moja na kwa wepesi kwa ukiukaji wowote wa heshima au haki zao.

[وَالَّذِينَ يَرْمُونَ الْمُحْصَنَاتِ ثُمَّ لَمْ يَأْتُوا بِأَرْبَعَةِ شُهَدَاء فَاجْلِدُوهُمْ ثَمَانِينَ جَلْدَةً]
“Na wanao wasingizia wanawake mahashumu, kisha wasilete mashahidi wanne, basi watandikeni bakora themanini.” [An-Nur 24:4]

عَنْ عَلْقَمَةَ بْنِ وَائِلٍ، عَنْ أَبِيهِ، أَنَّ امْرَأَةً، خَرَجَتْ عَلَى عَهْدِ النَّبِيِّ e تُرِيدُ الصَّلاَةَ فَتَلَقَّاهَا رَجُلٌ فَتَجَلَّلَهَا فَقَضَى حَاجَتَهُ مِنْهَا فَصَاحَتْ وَانْطَلَقَ فَمَرَّ عَلَيْهَا رَجُلٌ فَقَالَتْ إِنَّ ذَاكَ فَعَلَ بِي كَذَا وَكَذَا وَمَرَّتْ عِصَابَةٌ مِنَ الْمُهَاجِرِينَ فَقَالَتْ إِنَّ ذَلِكَ الرَّجُلَ فَعَلَ بِي كَذَا وَكَذَا . فَانْطَلَقُوا فَأَخَذُوا الرَّجُلَ الَّذِي ظَنَّتْ أَنَّهُ وَقَعَ عَلَيْهَا فَأَتَوْهَا بِهِ فَقَالَتْ نَعَمْ هُوَ هَذَا . فَأَتَوْا بِهِ النَّبِيَّ e فَلَمَّا أَمَرَ بِهِ قَامَ صَاحِبُهَا الَّذِي وَقَعَ عَلَيْهَا فَقَالَ يَا رَسُولَ اللَّهِ أَنَا صَاحِبُهَا . فَقَالَ «اذْهَبِي فَقَدْ غَفَرَ اللَّهُ لَكِ». «وَقَالَ لِلرَّجُلِ قَوْلاً حَسَنًا». قَالَ أَبُو دَاوُدَ (يَعْنِي الرَّجُلَ الْمَأْخُوذَ)، وَقَالَ لِلرَّجُلِ الَّذِي وَقَعَ عَلَيْهَا «ارْجُمُوهُ» (رواه ابو داود)

Pindi mwanamke mmoja alipotoka katika zama za Mtume (saw) akitaka kuswali, akakutana na mwanamume mmoja akamshambulia na kumzidi nguvu kisha akakidhi haja yake kwake (akambaka). Akapiga mayowe na mwanamume huyo akaondoka, akatokewa na mwanamume mwengine akamwambia: mtu yule amenifanyia kadha na kadha. Kikatokea kikundi cha muhajirina akawaambia: mwanamume yule amenifanyia kadha na kadha. Wakaenda na kumkamata mwanamume yule ambaye walidhani kwamba ndiye aliyembaka na kumleta kwake. Naye akasema: ndio, huyu ndiye. Kisha wakaja naye kwa Mtume (saw). Na pindi alipotoa amri juu yake akasimama yule mwanamume (halisi) aliyembaka akasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, mimi ndiye niliyemtendea hilo. Mtume wa Mwenyezi Mungu akamwambia (mwanamke huyo): “Nenda zako, hakika Mwenyezi Mungu amekusamehe”. “Na akamwambia mwanamume huyo maneno mazuri” (Abu Dawud amesema: akimaanisha mwanamume aliyekamatwa kimakosa), na yule mwanamume halisi aliyembaka mwanamke huyo, alisema: “Mpigeni mawe hadi afe”. [Abu Dawud]

Wakati wa Khilafah ya Umar bin Al Khattab (ra), mwanamke mmoja alimtuhumu mwanawe Abu Shahmah kuwa alimbaka. Umar (ra) akamuuliza mwanawe kuhusu uhalifu huo, aliyekiri kutekeleza kitendo hicho. Aliadhibiwa vikali hapo kwa hapo huku mwanamke huyo hakuekewa kosa lolote kwa uhalifu huo.

• Jukumu lililowekwa na Uislamu juu ya wanaume la kuwa wasimamizi wa wake zao na watoto wao huwawajibisha kuwahifadhi na kuwalinda kutokana na madhara. Kuliko tu kuwa na wadhifa wa kuwatawala na kuwaamuru pekee, jukumu hili kubwa la usimamizi (qiwaamah) ni lile la uchungaji wa wake na ndugu wa kike. Hili pia hupunguza ghasia dhidi ya wanawake. ﴿ٱلرِّجَالُ قَوَّٰمُونَ عَلَى ٱلنِّسَآءِ﴾ “Wanaume ni wasimamizi wa wanawake.” [An-Nisa: 34]

• Uislamu umefafanua haki za mke juu ya mumewe na kunasibisha hadhi ya wanaume katika maisha haya ya duniani na akhera kwa kuwatendea wema wake zao na binti zao. Sheria na kanuni zote hizi hupunguza ukatili na unyanyasaji wa wanawake. وَعَاشِرُوهُنَّ بِالْمَعْرُوفِ “Na kaeni nao kwa wema.” [An-Nisa: 19]
Mtume (saw) amesema, «أَكْمَلُ الْمُؤْمِنِينَ إِيمَانًا أَحْسَنُهُمْ خُلُقًا وَخِيَارُكُمْ خِيَارُكُمْ لِنِسَائِهِمْ» “Muumini aliyekamilika imani yake ni yule aliye na tabia njema na wabora wenu ni wale walio wabora kwa wake zao.” [Tirmidhi]

Rekodi za mahakama kutoka kwa Khilafah Uthmaniyya zaonyesha kuwa waume walio wanyanyasa wake zao waliadhibiwa na dola hiyo, ikiwemo kufungwa jela wakati mwengine. Mahakimu aghlabu walimfanya mume kukubali sharti kuwa endapo atamnyanyasa tena mke wake, basi atatalikishwa pasi na mke kusalimisha haki zake za ndoa za kifedha.
“Maisha ya ndoa ni yale ya utulivu na usuhuba. Jukumu la mume juu ya mkewe (qiwaamah) ni lile la uchungaji, na sio la utawala …” (Kifungu cha 120, Kielelezo cha Katiba ya Al-Khilafah cha Hizb ut Tahrir)

• Khilafah itachukua hatua pana za kuhifadhi hadhi ya wanawake wake, ikiwemo hata kuandaa majeshi yake dhidi ya majeshi ya kigeni yanayo chafua au hata kuhatarisha kuchafua heshima yao, kwani hiki ndicho kiwango cha juu cha hifadhi ambayo utawala wa Kiislamu unaimudu kwa wanawake wa dola yake.
Katika karne ya 9 chini ya Khilafah Abbasiyya, wakati wa utawala wa Khalifah al-Mu’tassim Billah, mwanamke mmoja wa Kiislamu alitekwa nyara na kunyanyaswa na mwanajeshi wa Kirumi nchini Syria. Katika kujibu hujuma hii, Khalifah huyu alipeleka jeshi lenye nguvu hadi mji wa Amuriyyah nchini Uturuki, ngome imara ya Warumi ili kumuokoa mwanamke huyo. Hii ni licha ya makao makuu ya Khilafah kuwa mjini Baghdad wakati huo. Inaashiria umakini ambao Khilafah ilitilia maanani hifadhi ya hadhi ya wanawake wake.

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Dkt. Nazreen Nawaz**
**Mkurugenzi wa Kitengo cha Wanawake katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Vipi Khilafah Itakavyo Hifadhi Haki za Kisiasa za Wanawake



• Uislamu huwawajibisha wanawake kuwa na dori changamfu katika siasa za mujtama wao: kuchunga mambo ya Ummah wao, kuzungumza dhidi ya ukandamizaji na ufisadi, kuamrisha mema (Ma'ruf) na kukataza maovu (Munkar), na kuwahisabu watawala wao. Dalili za Kiislamu zinazo waamrisha Waislamu kuwa wachangamfu katika siasa zinawahusu wanaume na hali kadhalika wanawake.

(وَالْمُؤْمِنُونَ وَالْمُؤْمِنَاتُ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاء بَعْضٍ يَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنكَرِ)

"Na Waumini wanaume na Waumini wanawake wao kwa wao ni marafiki walinzi …" [At-Taubah: 71]

Mtume (saw) amesema,

كَلاَّ وَاللَّهِ لَتَأْمُرُنَّ بِالْمَعْرُوفِ وَلَتَنْهَوُنَّ عَنِ الْمُنْكَرِ وَلَتَأْخُذُنَّ عَلَى يَدَىِ الظَّالِمِ وَلَتَأْطُرُنَّهُ عَلَى الْحَقِّ أَطْرًا وَلَتَقْصُرُنَّهُ عَلَى الْحَقِّ قَصْرًا

"Hapana, Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, hamutaacha kuamrisha mema na hamutaacha kukataza maovu, na wala hamutaacha kuzuia mikono ya dhalimu, na wala hamutaacha kumlazimisha juu ya haki na kumfunga sawa sawa na haki, isipokuwa Mwenyezi Mungu atazigonganisha nyoyo za baadhi yenu dhidi ya wengine, na atawalaani kama alivyo walaani wao." [Abu Dawud]

• Wanawake wana haki sawa za kisiasa kama wanaume chini ya Khilafah.

"Raia wote wa Dola watatendewa usawa bila ya kujali dini, jinsia, rangi au jambo jengine lolote. Dola imeharamishwa kubagua miongoni mwa raia wake katika mambo yote …" (Kifungu cha 6, Kielelezo cha Katiba ya Al Khilafah cha Hizb ut Tahrir)

• Kuhisabu na uwazi ni nguzo msingi za utawala wa Kiislamu. Hivyo basi Khilafah itawapa wanawake njia kadha wa kadha ili kutoa malalamishi dhidi ya dola au kumhisabu mtawala. Itawarahisishia na kuwashajiisha katika kudhihirisha rai zao za kisiasa.

"Kuwataka watawala kuhisabiwa kwa vitendo vyao ni haki kwa Waislamu pamoja na faradhi ya kutoshelezana (fardh kifaayah) juu yao." (Kifungu cha 20, Kielelezo cha Katiba ya Al Khilafah cha Hizb ut Tahrir)

• Nidhamu ya Kiislamu inawapa wanawake haki ya kuchagua wawakilishi wao na Khalifah. Hakika, Uislamu ndio nidhamu ya kwanza ulimwenguni kuwapa wanawake wake haki ya kuchagua kiongozi wao.

Wanawake wawili – Nusaybah bint Ka'ab Umm 'Amarah na Asma bint Amr ibn Adi – walikuwa ni miongoni mwa ujumbe wa Waislamu wa Yathrib katika Bay'ah ya Pili ya Al-Aqaba. Hii ilikuwa ahadi ya usaidizi wa kisiasa na ulinzi wa kijeshi aliopewa Mtume (saw), wakimkubali kama kiongozi wa dola yao.

Pindi Amr bin Al-'As (ra) alipokuwa akishauriana na raia wa Khilafah juu ya ni nani wanayempendelea kuwa kiongozi wao baada ya kifo cha Khalifah Umar bin Al-Khattab (ra), alitafuta maoni ya wanawake na wanaume vile vile.

"Mwanamke anaweza kuwachagua wanachama wa baraza la Ummah, na yeye mwenyewe kuwa mwanachama wake, na anaweza kushiriki katika uchaguzi wa Kiongozi wa Dola na kumpa ahadi ya utiifu (bay'ah)." (Kifungu cha 115, Kielelezo cha Katiba ya Al Khilafah cha Hizb ut Tahrir)

• Chini ya Khilafah wanawake wanaweza kuwa wanachama wa vyama vya kisiasa, kutoa maoni yao

*Endelea Uk..5*

katika vyombo huru vya habari, kuwa waandishi habari au kuasisi vyombo vya habari pasi na haja ya leseni.

• Wanawake watakuwa na haki ya kuchagua wawakilishi wa Baraza la Wilaya (Majlis Al-Wilayah) au Baraza la Ummah (Majlis Al-Ummah) yanayo shauri na kuhisabu mawali na Khalifah katika mambo yote ya dola.

“Kila raia wa Dola ana haki ya kuwa mwanachama wa Baraza la Ummah (Majlis al-Ummah), au Baraza la Wilaya … Hii ni kwa Muislamu na asiyekuwa Muislamu.” (Kifungu cha 107 Kielelezo cha Katiba ya Al Khilafah cha Hizb ut Tahrir)

• Katika Uislamu, maoni ya kisiasa ya wanawake huthaminiwa.

Mtume (saw) alitafuta ushauri na kuchukua ushauri wa mkewe Umm Salamah (ra) alipokabiliwa na mgogoro mbaya wa kisiasa katika Mkataba wa Hudaibiyah. Umar bin Al-Khattab (ra), Khalifah wa pili wa Uislamu alikuwa akiwakusanya wanaume na wanawake msikitini na kutafuta rai zao juu ya mambo kadha wa kadha. Pia angetafuta ushauri wa mwanamke anayeitwa Al-Shifa bint Abdullah juu ya mambo kadha wa kadha ya kisiasa kutokana na maarifa yake na upeo wake wa ufahamu, aghlabu akifadhilisha rai zake juu ya wengine.

Katika jumuiko moja la umma wakati wa utawala wa Umar bin Al-Khattab (ra) alipokuwa akiwaamrisha watu kutoweka viwango vya juu vya mahari katika ndoa, mwanamke mmoja ajuza alipambana na Khalifah wazi wazi katika rai zake, akipaaza sauti, “Umar! Huna haki ya kuingilia katika jambo ambalo Mwenyezi Mungu (swt) tayari ashalipitisha katika Qur’an”, akisoma ayah katika Surah An-Nisa, ayah ya 20 ili kuthibitisha hoja yake. Khalifah huyo akajibu, “Mwanamke huyu yuko sahihi na Umar amekosea”, na akaondoa amri yake.

Nafisa Bint Hasan alikuwa mwanachuoni maarufu wa karne ya 9 nchini Misri chini ya Khilafah ya Abbasiya. Alihusika pakubwa katika siasa za mujtama wake kiasi ya kuwa pindi watu walipokuwa na mizozo na wali wa Misri wangemtaka kutatua hali hiyo na kuhakikisha kupatikana kwa haki zao.

• Khilafah itawawezesha wanawake kuchukua malalamishi dhidi ya watawala au maafisa wa dola hadi Mahakama ya madhalim (Mahkamat ul-Madhalim), mahakama maalumu inayo chunguza utepetevu au dhulma katika utawala, ikiwaruhusu wanawake kuwahisabu waziwazi watawala wao bila ya hofu.

“Kadhi wa Mahakama ya Madhalim huteuliwa ili kuondoa vitendo vyote vya dhulma, vinavyofanywa na Khalifah, (ma)wali au afisa yeyote wa Dola, ambavyo vimetendewa yeyote …” (Kifungu cha 87, Kielelezo cha Katiba ya Al Khilafah cha Hizb ut Tahrir)

Ma’moon Ar-Rashid, mmoja wa Makhalifah wa Abbasiya, alikuwa akitenga siku za Jumapili kwa ajili ya hadhara ya umma ili kusikiza malalamishi yao. kuanzia asubuhi mapema hadi mchana, kila mmoja – wanaume na wanawake – walikuwa huru kuwasilisha malalamishi yao kwa Khalifah ambayo yalishughulikiwa mara moja. Siku moja mwanamke mmoja ajuza masikini alilalamika kuwa mtu mmoja dhalimu amempokonya mali yake. “Mtu huyo ni nani?” Khalifah aliuliza. “Ameketi ubavuni mwako,” mwanamke huyo ajuza akajibu, akimulekezea mtoto wa Khalifah, Abbas. Abbas akajaribu kutetea kitendo chake kwa sauti ya kusitasita huku mwanamke huyo ajuza akiendelea kupaza sauti katika manung’uniko yake. Khalifah akataja kuwa ni kutokana na ukweli wa kesi yake uliomfanya (mwanamke huyo) kuwa mkakamavu na kutoa uamuzi kwa manufaa yake.

• Kwa mujibu wa nass za Kiislamu, mwanamke hawezi kuwa mtawala katika Khilafah lakini hili kwa vyovyote vile kamwe haliingilii uwezo wake wa kujihusisha kikamilifu katika siasa za mujtama wake. Fauka ya hayo, Uislamu hautazami kuwa mtawala kama haki ya au fadhila bali jukumu kubwa lililofungamana na hisabu nzito kesho Akhera. Lakini mwanamke anaweza kuwa afisa au mwakilishi wa dola katika wadhifa usio wa kiutawala, kama vile mkuu wa kitengo au msemaji.

**لَمَّا هَلَكَ كِسْرَى سَأَلَ رَسُولِ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم: «مَنِ اسْتَخْلَفُوا؟» قَالُوا: بِنْتَهُ. قَالَ: «لَنْ يُفْلِحَ قَوْمٌ وَلَّوْا أَمْرَهُمُ امْرَأَةً**

Pindi Kisra alipokufa, Mtume (saw) aliuliza: “Ni nani aliyechukua wadhifa wake?” wakasema: binti yake. Akasema: “Watu wanaomtawalisha mwanamke mambo yao kamwe hawatafaulu.”

“Raia yeyote wa dola, mwanamume au mwanamke, Muislamu au asiyekuwa Muislamu, aliye na uwezo stahiki aweza kuteuliwa kama mkuu au mtumishi wa umma wa idara, halmashauri au kitengo chochote.” (Kifungu cha 98, Kielelezo cha Katiba ya Al Khilafah cha Hizb ut Tahrir)

“Inaruhusiwa kwa mwanamke kuteuliwa katika nyadhifa za utumishi wa umma na mahakama isipokuwa Mahakama ya Madhalim.” (Kifungu cha 115, Kielelezo cha Katiba ya Al Khilafah cha Hizb ut Tahrir)

• Hivyo basi Khilafah inasimama kama mwakilishi wa kweli wa haki za kisiasa za wanawake. Itawawezesha kujihusisha kisiasa kikamilifu katika mujtama, ambapo wamenyimwa hilo kwa muda mrefu chini ya tawala za kiimla na nidhamu zilizotungwa na binadamu katika ulimwengu wa Kiislamu.

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Dkt. Nazreen Nawaz**
**Mkurugenzi wa Kitengo cha Wanawake katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Vipi Khilafah Itakavyo Wadhamini Wanawake Haki Zao za Kielimu



Uislamu hutazama utafutaji elimu ya Kiislamu kuwa faradhi kwa wanawake na wanaume.

Mtume (saw) amesema, «طَلَبُ الْعِلْمِ فَرِيضَةٌ عَلَى كُلِّ مُسْلِمٍ» “Utafutaji elimu ni faradhi kwa kila Muislamu.” [Ibn Majah]

Kutilia maana hali ya juu kwa Mtume (saw) umuhimu wa elimu ya wanawake kumeashiriwa na usomi wa wengi wa wakeze, maswahaba wa kike wa Mtume (saw) (Sahabiyyat), na wanawake wengineo katika zama za utawala wake mjini Madina.

Aisha mke wa Mtume (saw) alipata lakabu ya ‘Faqihi wa kike wa Ummah’ (Faqihat ul Ummah) kutokana na elimu yake ya Hadith na ujuzi katika fiqh ya Kiislamu. Alisimulia zaidi ya Hadith 2200 kutoka kwa Mtume (saw). Aisha (ra) pia alikuwa mwanachuoni mkubwa wa utabibu, fasihi na mashairi.

Mtume (saw) angewafunza wanaume na wanawake kuhusu Uislamu msikitini na katika mijumuiko mingine ya umma. Vilevile alitenga siku moja kila wiki kuwaelimisha wanawake pekee kuhusu Dini yao. Mtume (saw) pia aliweka umuhimu juu ya wanawake kujua kusoma na kuandika, unaoashiriwa katika agizo lake kwa Shifa bint Abdullah la kumfundisha mkewe Hafswa jinsi ya kuandika.

Abu Sa’id al-Khudri (ra) ameripoti kuwa baadhi ya wanawake walimwambia Mtume (saw),

قَالَتِ النِّسَاءُ لِلنَّبِيِّ صلى الله عليه وسلم غَلَبَنَا عَلَيْكَ الرِّجَالُ، فَاجْعَلْ لَنَا يَوْمًا مِنْ نَفْسِكَ. «فَوَعَدَهُنَّ يَوْمًا لَقِيَهُنَّ فِيهِ، فَوَعَظَهُنَّ وَأَمَرَهُنَّ»

“Wanaume wametushinda (katika kupata elimu). Basi tujaaliye nasi siku yako moja ili nasi tufaidike vilevile. Mtume (saw) akaweka miadi nao siku moja ambayo angekutana nao, na angewapa mawaidha na kuwaelimisha kuhusu amri za Mwenyezi Mungu (swt). [Al-Bukhari]

Uislamu pia unawashajiisha wanaume na wanawake kuusoma ulimwengu unaowazunguka na kuleta manufaa kwa wanadamu katika nyanja zote – ikiwemo sayansi, utabibu, viwanda na teknolojia.

Ni utiliaji maanani huu mkubwa wa Uislamu kwa utafutaji elimu ya Kiislamu na aina nyenginezo za elimu unaoweka msingi kwa Khilafah kutambua umuhimu wa elimu ya wanawake.

Mtume (saw) asema,

وَمَنْ سَلَكَ طَرِيقًا يَلْتَمِسُ فِيهِ عِلْمًا سَهَّلَ اللَّهُ لَهُ بِهِ طَرِيقًا إِلَى الْجَنَّةِ

“Na mwenye kufuata njia katika kuitafuta elimu Mwenyezi Mungu humsahilishia kwa hilo njia ya kwenda Peponi.” [Muslim]

Khilafah huitazama elimu kama haki msingi kwa kila mtu binafsi na vilevile dharura kwa maendeleo ya kijamii na kimada katika mujtama wowote. Imewajibishwa kutoa elimu bila malipo katika viwango vya msingi na upili kwa wavulana na wasichana. Hii hujumuisha masomo kama

*Endelea Uk..7*

fanni za Kiislamu, Lugha ya Kiarabu, hesabu, na sayansi za utafiti kama bayolojia, kemia na fizikia. Dola pia itajizatiti kufadhili elimu ya juu bila malipo kwa wanaume na wanawake kwa kadri ya uwezo wake.

"Ni jukumu la Dola kumfundisha kila mtu, mwanamume au mwanamke, vile vitu ambavyo ni muhimu katika maisha ya kawaida. Hii yapaswa kuwa wajibu na kutolewa bila malipo katika viwango vya elimu ya msingi na upili." (Kifungu cha 178 cha Kielelezo cha Katiba ya Al-Khilafah cha Hizb ut Tahrir)

Ufundishaji wanafunzi wa kiume na wa kike katika shule za dola na za kibinafsi utakuwa kando kando.

Chini ya Khilafah, wavulana na wasichana, wanaume na wanawake wana haki sawa za kielimu. Ubaguzi wowote wa kijinsia au wa raia wake yeyote katika kupata elimu bora umeharamishwa. Fauka ya hayo, wanawake kama ilivyo kwa wanaume wanahitaji kupata elimu ya Kiislamu inayohitajika kuhusiana na maisha ya kisiasa, kiuchumi na kijamii pamoja na mambo mengine ili waweze kutimiza majukumu yao ya Kiislamu, kujihusisha na amali kadha wa kadha za kimujtama na vitendo ambavyo Uislamu umeviruhusu, na kujifunga na hukmu za Kiislamu kama Waislamu na kama raia wa dola. Hivyo basi Khilafah itawajibika kupangilia nidhamu yake ya kielimu ili kuwapa wasichana na wanawake elimu kama hiyo na pia kujizatiti kuondoa taasubi zozote za kimila au vizingiti vya kitamaduni vinavyo dunisha elimu ya wanawake au kuwazuia wasichana kutokana na kutafuta haki zao za kielimu.
"Wanawake wana haki na majukumu sawa kama wanaume, isipokuwa yale yaliyo fafanuliwa na dalili za Kisheria kuwa ya kiume na ya kike. Hivyo basi, mwanamke ana haki ya kufanya biashara, ukulima, na viwanda; kushiriki katika mikataba na miamala; kumiliki aina zote za mali; kuwekeza utajiri wake ima kibinafsi au kupitia wakala, na kutekeleza kibinafsi mambo yote ya kimaisha." (Kifungu cha 114 cha Kielelezo cha Katiba ya Al-Khilafah cha Hizb ut Tahrir)

Daima dola itajizatiti kuwa dola inayo ongoza duniani katika sayansi, utabibu; teknolojia, viwanda na nyanja nyinginezo kama inavyo wajibishwa na Uislamu, utaisukuma ili kutafuta ubora katika elimu. Hivyo basi itawashajiisha wanawake kuingia katika masomo ya juu na kuwarahisisishia katika uteuzi wa taaluma katika nyanja tofauti tofauti, ikiwemo fanni za Kiislamu, utabibu, sayansi, lugha na uhandisi. Yote haya yataimarisha matarajio ya kielimu ya wasichana na wanawake.

Ni wajib juu ya Khilafah kutoa elimu na huduma za matibabu bora zaidi iwezekanavyo kwa raia wake, kwani Mwenyezi Mungu (swt) ameisifu elimu kuwa 'Msimamizi' na 'Mchungaji' wa watu. Hivyo basi ipo haja ya kuwa na madaktari, wauguzi na walimu wa kike wa kutosha ili kutimiza dori hizi.

Ni katika mazingira haya ya masomo yaliyo wekwa kupitia utabikishaji wa nidhamu ya Kiislamu ndiyo yaliyo hakikisha kuwa elimu ya wanawake imenawiri chini ya Khilafah iliyopita kama itakavyo fanya tena Khilafah inayokuja InshaAllah.

"Mohammed Akram (mwanachuoni wa Kiislamu wa Kihindi wa zama hizi) alianza miaka minane iliyopita kuandika kamusi ya mjaladi mmoja ya wasifu wa maisha ya wanachuoni wa kike wa Hadith, mradi uliomfanya kupekua kamusi za wasifu, vitabu vya kale, rekodi na barua za madrasa kwa ajili ya kupata vyanzo stahiki. 'Nilidhani labda ningepata wanawake 20 au 30,' alisema. Mpaka kufikia sasa, amepata wanawake 8,000, kutokea miaka 1,400 iliyopita, na kamusi yake sasa imefikia mijaladi 40 …" (Kipande hiki kimevuliwa kutoka Makala "A Secret History" yaliyo andikwa na Carla Power yaliyo chapishwa katika Jarida la New York, Februari 25, 2007)

Mifano ya wanawake waliofaulu katika nyanja tofauti tofauti za masomo chini ya Khilafah:

Lubna wa Andalus (karne ya 10 Miladi) – Malenga aliye bobea katika nahau, balagha, hesabu na uandishi. Alikuwa mmoja wa waandishi wa dola na aliaminiwa na uandishi wa barua rasmi.

Fakhr al-Nisa Umm Muhammad Shuhdah (karne ya 12 Miladi) – Mtaalamu katika uandishi. Alikuwa akimuandikia Khalifah al-Muqtafi. Yasemekana kuwa katika wakati wake hakukuwa na mtu yeyote mjini Baghdad aliye lingana naye katika ubobeaji wake wa uandishi.

Mpasuaji wa Kituruki wa karne ya 15 Serefeddin Sabuncuoglu amewasifu wapasuaji wa kike mjini Anatolia kutekeleza taratibu za upasuaji kwa wangonjwa wa kike.

Labana wa Kurtuba (karne ya 10 Miladi) – Mjuzi katika hesabu na fasihi. Alikuwa na uwezo wa kutatua hesabu ngumu kabisa za kijometriki na aljebra. Elimu yake pana ya fasihi jumla ilimpa ajira ya kuwa katibu wa Khalifah, al-Hakem II.

Maeriam "al-Astrolabiya" Al-Ijilya (karne ya 10 Miladi) – Mwanasayansi, mvumbuzi, mnajimu na muundaji wa vifaa vinavyotumika kutathmini kisimamo cha jua na sayari. Miundo yake ilikuwa na ubunifu sana kiasi cha kuajiriwa na mtawala wa mji alimoishi.

Zaynab kutoka kabila la Banu Awd (karne ya 10 Miladi) – Mjuzi katika utabibu, hususan katika kutibu vidonda na matatizo ya macho.

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Dkt. Nazreen Nawaz**
**Mkurugenzi wa Kitengo cha Wanawake katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Vipi Khilafah Itakavyo Unda Nidhamu ya Elimu ya Daraja ya Juu Kabisa



Allah (swt) asema,

(الٓر كِتَابٌ أَنزَلْنَاهُ إِلَيْكَ لِتُخْرِجَ النَّاسَ مِنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ بِإِذْنِ رَبِّهِمْ إِلَى صِرَاطِ الْعَزِيزِ الْحَمِيدِ)

"Alif Lam Ra. (A. L. R) Hichi ni Kitabu tulicho kiteremsha kwako ili uwatowe watu kwenye giza uwapeleke kwenye muwangaza, kwa idhini ya Mola wao Mlezi, uwafikishe kwenye Njia ya Mwenye nguvu, Msifiwa." [Ibrahim: 1]

• Ili kuunda Nidhamu ya Elimu ya Daraja ya Juu Kabisa ya aina hiyo yahitaji nidhamu ya kisiasa ya daraja ya juu kabisa – nidhamu inayo kumbatia ruwaza ya kisiasa ya kipekee, ya hali juu na huru kwa dola yake na kwa ulimwengu, iliyo jengwa kwa msingi wa ayah hiyo ya juu – kuwatoa watu kutoka katika giza la ujinga wa ukafiri na kuwapelekea katika nuru ya Uislamu na uadilifu na mafanikio unayoleta kwa wanadamu katika kila nyanja ya maisha – kiroho, kiakili, kiakhlaqi, kisiasa, kiuchumi, na katika sayansi na teknolojia.

Nidhamu hii ya kisiasa ya daraja ya juu kabisa ni Khilafah kwa njia ya Utume inayo tabikisha imani, sheria na nidhamu za Kiislamu kwa ukamilifu juu ya dola, na ambayo kwa karne kadhaa iliongoza dunia katika mafanikio ya taasisi zake za kielimu na ubunifu na uvumbuzi wake wa kipekee, pamoja na mchango wake mkubwa kwa maendeleo ya binadamu.

• Khilafah itaasisi nidhamu ya elimu ya daraja ya juu kabisa iso na kifani itakayo kuza kizazi cha vijana na kuunda Ummah na dola zinazojifunga na sifa za kuwaongoza wanadamu kutoka katika giza kwenda katika nuru kama inavyo amrishwa na Mwenyezi Mungu (swt). Haitakubali kubaki nyuma ya mataifa mengine katika mafanikio ya kimasomo wala kukubali daraja yoyote ya pili ya nidhamu ya elimu inayofadhiliwa na makombo kutoka kwa dola.

• Khilafah inawajibishwa na Mwenyezi Mungu (swt) kuwa na ruwaza huru ya kisiasa kindani na kimataifa iliyo jengwa kwa msingi safi juu ya Uislamu; na hivyo pia kuwa huru katika uundaji wa mtaala wake wa elimu, pamoja na utoaji huduma zake za umma na miundo msingi, na ushibishaji mahitaji ya dola na watu wake. Hivyo basi haitakubali kutegemea biladi yoyote ya kigeni katika kuimarisha sekta zake za uchumi, ukulima, viwanda, matibabu, elimu, jeshi, sayansi na teknolojia au sehemu nyengine yoyote ya dola ambayo huianika wazi kwa utumiwaji vibaya na serikali za kikoloni.

• Khilafah itaasisi ndoa imara kati ya elimu na utekelezaji wa kadhia na maslahi nyeti ya dola na raia wake, ikihakikisha kujitegemea na kujitosheleza – hivyo kuondoa utengano uliopo sasa kati ya nidhamu za elimu katika biladi zetu na mahitaji ya kiviwanda, kiukulima, kiufundi na mahitaji mengineyo ya mujtamaa zetu, inayopelekea kutegemea mataifa mengine. Hili, pamoja na uwekezaji mzito wa Khilafah katika uimarishaji viwanda ili kukidhi mahitaji ya mujtama wake kwa kujitegemea yenyewe na kuifanya dola hiyo kuwa dola kuu duniani, itadhibiti na kutumia ujuzi na akili za kipekee za wahitimu vyuo wa Ummah huu kwa ajili ya maendeleo ya dola hii, ili uwezo wao mwanana usifujwe au kutekwa nyara na serikali za kigeni.

• Msingi unaofunga vipengee vyote vya nidhamu ya

***Endelea Uk..9***

elimu ndani ya Khilafah – kuanzia malengo yake, masomo yanayo fundishwa, maalumati yaliyomo ndani ya mtaala na mafunzo, mpangilio wa shule na kila kitu chengine ni Itikadi ya Kiislamu pekee, kwani Mwenyezi Mungu (swt) asema,

(وَمَن يَبْتَغِ غَيْرَ الإِسْلاَمِ دِينًا فَلَن يُقْبَلَ مِنْهُ وَهُوَ فِي الآخِرَةِ مِنَ الْخَاسِرِينَ)
"Na anayetafuta dini isiyokuwa Uislamu haitakubaliwa kwake. Naye Akhera atakuwa katika wenye kukhasiri." [Al-e-Imran: 85]

"Ni wajib kuwa Itikadi ya Kiislamu iwe ndio msingi wa mtaala wa elimu. Mtaala na mbinu za ufundishaji zote hutungwa kwa njia isiyo potoka kutoka katika msingi huu." (Kifungu cha 170, Kielelezo cha Katiba ya Al-Khilafah cha Hizb ut Tahrir)

• Kuna malengo matatu makuu ya Nidhamu ya Elimu ya Khilafah:

(i) Uundaji Shakhsiya ya Kiislamu:

Hili hupatikana kupitia kukuuza Itikadi, fahamu na tabia za Kiislamu ndani ya wanafunzi ili wawe ni Waislamu wanaouchukua Uislamu kuwa ndio msingi wa pekee wa fikra, maamuzi, matamanio na vitendo vyao vyote na kuunda maisha yao yote kwa mujibu wa Dini yao. Lengo hili litasaidiwa na mazingira ya Kiislamu ya Khilafah ambapo vyombo vyake vya habari, misikiti na taasisi zote nyengine hazitapigia debe chochote isipokuwa fahamu safi za Kiislamu.

(ii) Ufundishaji Ujuzi na Elimu ya Kivitendo kwa Ajili ya Maisha:

Wanafunzi watafundishwa wanachohitaji katika ujuzi na elimu ya kuingiliana na mazingira yao ili kuwatayarisha kuingia katika mzunguko wa maisha ya kivitendo, kama vile hesabu, sayansi jumla na elimu na ujuzi wa kutumia ala na uvumbuzi, kwa mfano vifaa vya umeme na elektroniki, tarakilishi, vifaa vya nyumbani, ala za ukulima na viwanda, na kadhalika. Pia watafunzwa michezo yenye manufaa kama vile kuogelea na ulengaji shabaha, na baada ya kubaleghe watapewa mafunzo ya kijeshi chini ya ishrafu ya jeshi.

(iii) Utayarishaji Wanafunzi Kuingia Vyuo Vikuu:

Wanafunzi watatayarishwa kwa ajili ya kuingia vyuo vikuu kupitia kuwafundisha sayansi msingi zinazo hitajika – iwe za kithaqafa kama Fiqh, Lugha ya Kiarabu, au Tafsiri ya Qur'an, au sayansi za kiutafiti – kama vile hesabu, kemia, bayolojia au fizikia. Lengo ni kuunda shakhsiya, wanazuoni, wanasayansi, na wataalamu wa kipekee katika kila nyanja ya maisha ili kuimakinisha Khilafah kama dola kuu, yenye ushawishi, inayo ongoza duniani. Mbinu za ufundishaji zinazo shajiisha tafakari ya kina zitatumiwa. Sayansi za kiutafiti kwa mfano zitafundishwa kwa njia inayo jenga ujuzi wa kutathmini, na ambapo mada zitatumiwa ili kutatua matatizo halisi ya kimaisha na kufanyiwa utafiti ili kuvua manufaa kutokana nazo ili kutumikia maslahi ya Ummah na kadhia zake nyeti. Mjumuiko huu jumla wa mtaala wa ufundishaji utaunda mjumuiko jumla wa shakhsiya za Kiislamu zilizo za kipekee katika ufahamu wao wa Dini yao na maumbile ya ulimwengu huu, pamoja na kutayarishwa kwa msingi unao hitajika kuingia katika masomo ya juu.

• Daraja za usomaji shule pia zimeundwa juu ya Itikadi ya Kiislamu kwani zimefungwa kwa msingi wa dalili za Kisheria zinazo husiana na hukmu, majukumu, na adhabu tofauti tofauti za Kiislamu zinazo tekelezwa juu ya mtoto katika umri tofauti tofauti. Kuna daraja 3 za shule – ya kwanza (au daraja ya Msingi) – kuanzia umri wa miaka 6 hadi 10; daraja ya pili (au Shule ya Wastani) kuanzia kukamilisha umri wa miaka 10 hadi 14; na daraja ya tatu (au Shule ya Upili) kuanzia kukamilisha miaka 14 hadi mwisho wa daraja za shule.

• Hakutakuweko na mchanganyiko baina ya wanaume na wanawake katika taasisi za elimu za dola kama ilivyo fafanuliwa na Uislamu – ima baina ya wanafunzi au walimu.

• Ni jukumu la Kiislamu juu ya Khilafah kutoa ubora wa hali ya juu wa elimu kwa kila mmoja wa raia wake kama haki msingi – bila ya kujali dini, tabaka, jinsia au kiwango chao cha utajiri. Inawajibishwa kuweka shule za kutosha za msingi na upili na kuajiri walimu wa kutosha kwa raia wote wa dola na kuwapa vifaa vyote wanavyo hitaji ili kufikia malengo ya sera ya elimu bila ya malipo.

"Ni jukumu juu ya Dola kumsomesha kila mtu, mwanamume au mwanamke, vile vitu ambavyo ni muhimu katika maisha ya kawaida. Hili lapaswa kuwa wajib na kupeanwa bila ya malipo katika viwango vya elimu ya msingi na upili. Dola inapaswa, kwa kadri ya uwezo wake, kutoa fursa kwa kila mmoja kuendelea na elimu ya juu bila ya malipo." (Kifungu cha 178, Kielelezo cha Katiba ya Al-Khilafah cha Hizb ut Tahrir)

• Uwekezaji katika elimu utakuwa ndio kipaumbele cha Khilafah. Kama dola inayo tafuta kuongoza dunia na kuwatumikia watu wake na wanadamu wote kwa jumla kwa ikhlasi, haitakubali nidhamu yoyote ya elimu ya daraja ya pili kutokana na ukosefu wa ufadhili. Bali, itatafuta kuunda wingi wa walimu na wahadhiri walio funzwa vyema na wenye kulipwa vizuri, pamoja na shule, vyuo, vyuo vikuu, vituo vya utafiti, maktaba, maabara na nyengine zaidi za kisasa, zenye vifaa vya kutosha, kwa kutumia mali ya Hazina yake Kuu (Bait ul-Mal), ambayo mali zake inshaAllah zitakuwa nyingi mno kutokana na umbile sahihi la nidhamu ya kiuchumi ya Khilafah. Dola itamsaidia kila mwanafunzi wa kiume na wa kike kufikia uwezo wake kamili bila ya kujali utajiri wao na kuwasaidia kufika kiwango cha juu zaidi cha usomi na ubunifu ili kuzalisha wingi wa mujtahidina, wanasayansi, na wavumbuzi wa kipekee InshaAllah.

Endelea Uk..10

“Dola hupeana maktaba na maabara na njia zote za elimu nje ya shule na vyuo vikuu, ili kuwawezesha wale wanaotaka kuendeleza utafiti wao katika nyanja tofauti tofauti za elimu, kama fiqh, Hadith na tafsiri ya Qur’an, fikra, utabibu, uhandisi na kemia, uvumbuzi, utambuzi, nk. Hili hufanywa ili kuunda ndani ya Ummah mujtahidina wengi zaidi, wanasayansi na wavumbuzi wa kipekee.” (Kifungu cha 179, Kielelezo cha Katiba ya Al-Khilafah cha Hizb ut Tahrir)

• Katika ruwaza ya Khilafah ya Elimu ya Juu, kuna ndoa ya karibu baina ya nidhamu ya elimu ya dola na utekelezaji mahitaji ya mujtamaa. Kwa mfano, mojawapo ya malengo ni kuimarisha shakhsiya ya Kiislamu ya wanafunzi wa elimu ya juu ili kuwafanya kuwa viongozi wanao linda na kutumikia kadhia nyeti za Ummah, kama vile kuhakikisha utabikishaji sahihi wa Uislamu, kuuhisabu uongozi, kubeba ulinganizi, na kupambana na matishio ya umoja wa Ummah, Dini au Khilafah. Hii yamaanisha kuwa thaqafa ya Kiislamu inafundishwa kwa njia ya kuendelea kwa wanafunzi wa elimu ya juu, bila ya kujali taaluma zao walizo chagua. Khilafah pia itashajiisha na kutoa njia za wanafunzi kuchukua taaluma katika nyanja zote za thaqafa ya Kiislamu ili kuzalisha wanazuoni, viongozi, makadhi na mafuqaha wa dola wa siku za usoni ili Ummah uendelee katika utabikishaji, kuhifadhi, na kueneza Dini yao.

• Elimu ya juu pia inatafuta kuzalisha majopo kazi yaliyo na uwezo wa kuchunga maslahi nyeti ya Ummah kama vile kuhifadhi chakula bora na cha kutosha, maji, makao, usalama na matibabu kwa watu, pamoja na kuzalisha madaktari, wahandisi, walimu, wauguzi, wakalimani na wataalamu wengine wa kutosha ili kuchunga mambo ya Ummah. Hili litajumuisha uzalishaji wa wajuzi ambao watachora mipango ya muda mfupi na muda mrefu na kubuni njia na mbinu za kisasa kwa ajili ya maendeleo ya ukulima, viwanda na usalama ili kuiwezesha dola kujitosheleza yenyewe katika kusimamia mambo yake.

• Hivyo basi nidhamu ya elimu ya Khilafah itakuwa ya kipekee, maridadi na isiyo mithili katika umbile lake. Hakika, nidhamu hii ya Kiislamu iliyozaa viongozi wa ajabu kama vile Umar bin Al-Khattab (ra), Umar bin Abdul Aziz, na Harun al Rashid; na wanazuoni wa kipekee kama vile Ash-Shafi, Ibn Taymiyyah, na Nafissa bint Hassan (rm); na wanasayansi maarufu kama vile Ibn Sina, Al-Khwarizmi, na Mariam Al-Astrolabiya’ Al-Ijliya – kwa mara nyengine tena itazaa viongozi, mujtahidina, na wabunifu wa kisayansi wa kipekee kwa Ummah huu inshaAllah – ikizalisha kizazi na hadhara ya dhahabu.

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Dkt. Nazreen Nawaz**
**Mkurugenzi wa Kitengo cha Wanawake katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Vipi Khilafah Itakavyo Kuwa Dola Inayo Ongoza Katika Sayansi na Teknolojia



Mapinduzi ya kiviwanda 4.0 yalitangazwa kama ajenda ya kiulimwengu katika Kongamano la Kiuchumi la Kiulimwengu la mwaka 2016, yaliwasili kama mafuriko makubwa katika biladi nyingi za Waislamu. Kuanzia mapinduzi ya kiviwanda 1.0 ambayo yalijiri katikati mwa karne ya 18 ambapo kuzuka kwa mitambo ya kutumia bukhari yalibadilisha (matumizi ya) wanyama wakati huo na kufanya mabadiliko ya kimsingi, hususan kwa uchumi wa kiulimwengu. Yakaendelea kwa kuja mapinduzi ya kiviwanda 2.0 yaliyojitokeza kwa kuja mitambo ya nguvu za umeme na magari ya utumizi wa nguvu za mafuta. Uvumbuzi huu ulichochea kuzuka kwa simu, magari, ndege, nk. vilivyo badilisha pakubwa sura ya ulimwengu. Katikati mwa miaka ya 80 hadi mwanzoni mwa miaka ya 2000 ikawa ndio kudhihiri kwa mapinduzi ya kiviwanda ya tatu, hadi sasa yanapo ingia mapinduzi ya kiviwanda 4.0 ambapo maendeleo ya teknolojia ya mawasiliano ya tovuti na hata uhodari wa kubuniwa yamekuwa ni kitu ambacho sio ndoto tena.

Lakini maendeleo yote haya ya kiteknolojia kwa bahati mbaya yanadhibitiwa kikamilifu na wageni ambao msukumo wao mkubwa ni kaida ya kirasilimali, kwa jina KBE (uchumi uliojengwa kwa msingi wa elimu). Ulimwengu wa Kiislamu umekuwa tu ni bidhaa na masoko. Tafiti za vyuo vikuu katika biladi za Waislamu pia zinafanywa kuvitumikia viwanda vya kigeni ambavyo kihakika vinamilikiwa na warasilimali makafiri.

Matunda ya utafiti daima huenda sambamba na mahitaji ya viwanda yanayo hitaji ubunifu mkubwa. Hivyo, ndio maana kuwa ni vigumu kwa vyuo vikuu katika ulimwengu wa Kiislamu kuweza kupenya na kuingia katika orodha ya vyuo vikuu 100 vya kwanza ulimwenguni kwa kuwa karibu biladi zote za Waislamu zimekuwa zikikabiliwa na KUPOROMOKA KIVIWANDA kwa kiasi kikubwa, huku Wamagharibi wakiwa katika hatua ya maendeleo ya kiviwanda kwa zaidi ya miaka 150 iliyopita. Huku mojawapo ya mambo yanayo hitajika kwa dola kusemwa kuwa inaweza kumudu sayansi na teknolojia ni ikiwa ina uwezo wa kuunda nguvu ya utafiti inayo pelekea utatuzi wa matatizo yanayo kabiliwa na dola hiyo, pamoja na uwezo wa kuunda nidhamu ya viwanda yenye kutekeleza natija za utafiti huo.

Huku kinaya kikiwa, tangu kuvunjwa Khilafah, ulimwengu wa Kiislamu uliridhika kwa kiasi fulani na wadhifa wa “wafanyi kazi” na “watumizi” wa bidhaa nyingi na huduma za teknolojia zinazo nadiwa masokoni, zinazo miminika katika biladi za Waislamu. Makala haya yatajadili jinsi ruwaza ya Uislamu inavyo tekelezwa katika dola ya Khilafah katika kumudu sayansi na teknolojia katika zama za leo za kidijitali. Ruwaza na mpangilio ambao umesahauliwa na Waislamu wenyewe kwa muda mrefu.

**RUWAZA NA MKAKATI WA DOLA YA KHILAFAH**

Dhati ya dola katika Uislamu ni kulinda na kudumisha

*Endelea Uk..12*

roho, akili, dini, mali, izza, usalama na dola. Hivyo basi, siasa zote za kielimu na kiviwanda zitashirikishwa pamoja ili kupata yale yanayoitwa malego ya sheria (Maqaasid ul-Shari'ah), kama ilivyo fafanuliwa chini:

**A. Mkakati katika Kuunda Uwezo wa Dola katika Kuimudu Elimu na Teknolojia**

Mkakati wa kwanza umefungamanishwa na uundaji wa nidhamu saidizi tatu (3) zinazo saidia uwezo wa dola wa kumudu elimu ya juu kabisa.

1. Uundaji wa nidhamu ya elimu yenye maono kuanzia kiwango cha msingi, upili hadi cha elimu ya juu ambapo filosofia na utamaduni wa kisayansi hutafutwa kutoka katika Itikadi ya Kiislamu pekee, hivyo kizazi chenye sifa ya fikra ya uongozi na uaminifu kitazaliwa, kikiwa na ujuzi na nyanja za taaluma tofauti tofauti.

2. Uundaji wa nidhamu ya utafiti na maendeleo (R&D), ambayo ni uwezo wa kujumuisha utafiti kutoka kwa taasisi za utafiti za dola, vitengo, pamoja na kutoka kwa vyuo vikuu; ambapo zote zinadhibitiwa, kushajiishwa, na kufadhiliwa kikamilifu na dola.

3. Uundaji wa nidhamu ya mkakati wa kiviwanda inayo milikiwa na kusimamiwa huru na dola na kujengwa kwa msingi wa mahitaji ya kijeshi ya kisasa na ushibishaji wa mahitaji msingi ya watu. Uhuru wa viwanda ikiwemo uwezo wa kudhibiti, kusimamia na kuhakikisha usalama wa mahitaji ya vipengee muhimu vya viwanda, kwa majina: mali ghafi, teknolojia, ujuzi, uhandisi, fedha, uwezo wa kuunda silsila kamili ya kiviwanda, pamoja na sera.

Kuhusu elimu, Khilafah ya Kiislamu pamoja na upande wa siasa zake za kigeni na mkakati wa diplomasia itashirikiana kwa uchangamfu na nchi nyenginezo zisizo maadui. Yaweza kuwa ni katika ubadilishanaji walimu na wajumbe baina ya nchi hizi mbili katika kueneza thaqafa na lugha ya kila mojawapo. Kaida za makubaliano ya kimataifa ya Khilafah katika Elimu ni kama zifuatazo:

1. Khilafah hutabikisha mtaala wa elimu kwa sera maalumu ili kuunda shakhsiya ya Kiislamu (shakhsiyyah Islamiyah)

2. Sheria ya Kiislamu huwezesha amali za ufundishaji na usomaji ndani ya muundo wa kuimarisha elimu inayo nufaisha Ummah na ulimwengu.

3. Khilafah huenda ikafanya makubaliano ili kuleta walimu na wahadhiri katika nyanja ya sayansi za kiutafiti kutoka ng'ambo kwa sababu mwalimu amefungwa na mtaala wa dola na hapaswi kupotoka kutokana nao.

4. Imeharamishwa kufanya makubaliano ambayo ndani yake yanaruhusu nchi nyenginezo kueneza fikra na mfumo potofu, au kufungua shule za kibinafsi miongoni mwa Ummah wa Kiislamu.

5. Imeharamishwa kujifunga na makubaliano ambayo ndani yake yanaitaka Khilafah kujifunga na mpango wowote ambao hawendi sambamba na sera za elimu ambazo ni lazima zishikiliwe imara.

Kuhusu nidhamu ya kiviwanda, viwanda huelekezwa ili kuweza kutimiza mahitaji yote ya watu, Waislamu na wasio kuwa Waislamu, pia kuweza kukidhi mahitaji nyeti ya Dola, na kuweza kuunda uhuru wa nchi kwa kaida zifuatazo:

1. Nidhamu za viwanda zenye kuenda juu ya msingi wa nidhamu ya kiuchumi ya Kiislamu katika kaida za uwekezaji na umilikaji. Uislamu umefafanua kuwa baadhi ya rasilimali asili haziwezi kumilikiwa na watu binafsi, wanajeshi, sembuse wageni. Umilikaji ni wa Ummah mzima. Dola inakuwa msimamizi tu ili kutoa manufaa kamili kwa watu.

2. Sekta nyeti ya viwanda ni lazima idhibitiwe na dola, kama vile ukulima, madawa, kawi, usafiri, miundo msingi, na kadhalika. Maendeleo yote ya kiviwanda ni lazima yajengewe muundo huru. Hapapaswi kuwa na fursa hata ndogo itakayo tufanya kuwategemea makafiri, katika teknolojia (kupitia kanuni za utoaji leseni), uchumi (kupitia mikopo au usafirishaji- uagizaji bidhaa) na siasa. وَلَن يَجْعَلَ اللهُ لِلْكَافِرِينَ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ سَبِيلاً"... na wala Mwenyezi Mungu hatawapa makafiri njia ya kuwashinda Waumini. (TMQ An Nisa: 141)

3. Viwanda haviko kwa ajili ya usafirishaji bidhaa, isipokuwa wakati huo huo kwa ajili ya mahitaji msingi tofauti tofauti ya watu ni lazima kuagizwe.

4. Viwanda pia vinajengwa juu ya msingi wa mikakati ya da'wah na jihad, ya kujihami pamoja na kufungua, ya kimwili na isiyo ya kimwili. Viwanda vyote vilivyoko ni lazima viwe na uwezo wa kutoa mahitaji kwa ajili ya jihad vinapo hitajika. Viwanda vya vifaa vizito ambavyo katika wakati wa amani vitatengeza magari moshi au vyombo vya jikoni, wakati wa vita ni lazima viweze kubadilishwa kwa haraka kuwa viwanda vya vifaru na bunduki za otamatiki.

**B. Mkakati katika Kuchukua Elimu kutoka kwa Hadhara nyenginezo**

i. Ushirikiano wa kielimu, sayansi, na teknolojia pamoja na Dola za Kikafiri zilizo katika mkataba (Mu'ahid) Makubaliano katika uwanja wa sayansi na teknolojia yanaruhusiwa kikamilifu, kwa sababu sheria ya Kiislamu inayaruhusu kwa hilo. Hivyo basi, ushirikiano kama huo unaruhusiwa kulingana na aina ya ushirikiano, huku mandhari ya siasa za kimataifa ikiendelea kuzingatiwa.

ii. Dola Husalimisha Makundi ya Wanasayansi ili Kutafuta Elimu katika Nchi Maalumu.

*Endelea Uk..13*

Ni dola pamoja na upande wake wa kisiasa ndio itakayo yatuma makundi ya wanasayansi ili kusoma ng'ambo kwa ajili ya maslahi ya kistratejia ya Dola ya Khilafah. Hivyo pindi Khalifah alipoona kuwa ili kuboresha jihad dhidi ya dola kuu ya Kirumi yahitaji majeshi imara ya majini, alituma wajumbe wa Ummah wa Kiislamu ili kujifunza mbinu za ujenzi wa meli, usafiri pamoja na unajimu na mwelekeo wa maeneo, unga wa bunduki, na kadhalika. Na kwa haya ni lazima wajifunze kwa China – ambayo ni ya kwanza kujua kuhusu mwelekeo wa maeneo au unga wa bunduki – kisha wakaenda huko, ingawa safari ilikuwa ngumu, na ni lazima wajifunze lugha kadha wa kadha za kigeni.

iii. Kuwaajiri Wanasayansi wa Kigeni ili Kuufunza Ummah wa Kiislamu

katika hali fulani ya kisiasa, hatua za kijasusi huenda zikachukuliwa, hususan wakati wa kupambana na nchi maadui wa Khilafah ya Kiislamu, kama katika zama za Sultan Muhammad al-Fatih (1453 M) ambapo majaribio yalifanywa kumwacha huru mfungwa Orban, mjuzi, mhandisi, mtengezaji bunduki, kutoka gereza la Kostantiniya. Alifungwa na Mfalme Costantine ili kumzuia kuajiriwa na jeshi la Uthmaniya. Kufupisha hadithi, kwa hatua za umakini Orban aliachwa huru na kuja mbele ya Sultan Al-Fatih. Kisha aliajiriwa kwa mshahara wa juu zaidi ya mara kumi kuliko alipokuwa akifanya kazi mjini Kostantiniya. Hatimaye, bunduki kubwa ilitengezwa, ambayo ilikuwa mpya zaidi kwa wakati ule.

Kuunda upya izza ya Uislamu inawezekana kufanywa na ulimwengu wa Kiislamu endapo watakuwa na umoja kama hadhara ili iwe "nguvu mpya" katika mandhari ya kisiasa ya kiulimwengu. Ummah wa Kiislamu karibuni utaregea kuongoza hadhara ya kiulimwengu na maendeleo ya kiteknolojia, endapo ubora wa kizazi chao mara moja kitaelekezwa upya kuwa kizazi cha viongozi. Kwa sababu biladi za Waislamu zina nguvu kubwa mno za rasilimali watu na rasilimali za kiasili, ambazo, ikiwa zitaungana chini ya kivuli cha Khilafah, hakuna nchi au taifa litalingana nayo.

Hili kwa yakini linajibu utegemeaji wa Ummah wa Kiislamu juu ya teknolojia kutoka nchi za Magharibi. Siasa za ukiritimba wa elimu zinazo fanywa na Magharibi zitakabiliwa na Ummah wa Kiislamu kwa uhuru na mtazamo imara wa mfumo wao. Na polepole lakini kwa uhakika, msimamo utabadilika. Magharibi ndiyo itakayoitegemea Khilafah ya Kiislamu. InshaAllah.

*Wallahu A'lam bi-Suwab*

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Fika Komara**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb utTahrir**

# Vipi Khilafah Itakavyo Unda Familia Imara



• Nguvu na utulivu wa familia ya Waislamu wakati mmoja iliwahi kuwa sifa ya kipekee ya Ummah huu wa Kiislamu. Gaston Jezz, profesa wa Kiswizi wa kanuni ya familia aliye zuru Jamhuri ya Uturuki kufuatia kuvunjwa kwa Khilafah Uthmaniya alisema kuwa utulivu wa imani za kidini katika ardhi hii, "ulizalisha nyumba za familia imara zaidi ulimwenguni, na umbile hili liliasisi maisha ya umma ambayo kamwe hayajawahi kuonekana katika historia ya taifa lolote."

• Lakini, leo kuna mgogoro unaoathiri umoja wa familia ya Waislamu kutokana na mazingira ya maadili na sheria zisizo kuwa za Kiislamu zinazo tuzunguka sisi na jamii zetu chini ya nidhamu tunazoishi nazo kwa sasa na serikali zisizo kuwa za Kiislamu zinazo tutawala juu yetu. Nidhamu na serikali hizi zimemomonyoa vibaya ndoa, kuvuruga cheo cha mama, na kuchochea kuvunjika kwa familia kupitia sheria na sera zao haribifu.

• Hivyo basi, ili kujenga familia imara, yahitaji mabadiliko ya mizizi na matagaa ya nidhamu za kisiasa katika ardhi zetu, na mageuzi kamilifu ya msingi, maadili na sheria ndani ya mujtama zetu, kupitia kusimamisha dola inayo tambua umuhimu mkubwa wa kulinda utukufu wa ndoa, kunyanyua hadhi ya cheo cha mama na kujenga na kuhifadhi familia nzuri. Hili lapaswa kujitokeza kupitia misingi, sheria na nidhamu zake ambazo zitaileta kivitendo ruwaza hii njema katika uhalisia. Ruwaza hii kubwa yaweza kupatikana pekee kupitia dola iliyo jengwa juu ya msingi safi wa Itikadi ya Kiislamu inayo tabikisha kwa ukamilifu sheria ZOTE za Kiislamu – kwani ni Mwenyezi Mungu (swt) pekee, Mjuzi wa kila kitu, Mwenye hekima, Anayejua vizuri zaidi namna ya kupangilia mambo ya wanaume na wanawake, haki na majukumu yao katika njia itakayo leta furaha na mafanikio kwa familia na wanafamilia wake wote. Mwenyezi Mungu (swt) asema,

إِنَّمَا كَانَ قَوْلَ الْمُؤْمِنِينَ إِذَا دُعُوا إِلَى اللَّهِ وَرَسُولِهِ لِيَحْكُمَ بَيْنَهُمْ أَن يَقُولُوا سَمِعْنَا وَأَطَعْنَا وَأُولَٰئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ

"Haiwi kauli ya Waumini wanapoitwa kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake ili ahukumu baina yao, ila ni kusema: Tumesikia, na tumetii! Na hao ndio wenye kufanikiwa." [An-Nur: 51]

• Dola hii iliyo jengwa kwa msingi safi wa Uislamu na inayo tabikisha imani, maadili na sheria zake zote ni Khilafah kwa njia ya Utume – Nidhamu ya Mwenyezi Mungu (swt). Uongozi huu wa Kiislamu utageuza misingi na sheria tukufu za kijamii na kifamilia za Kiislamu kutoka kwa mkusanyiko wa majukumu na hukmu zinazo fuatwa na Waislamu wachache wachamungu hadi kwa mkusanyiko wa maadili na sheria ambazo zitakuwa ndio ada ya mujtama mzima, zinazo tabanniwa na wengi

***Endelea Uk..15***

miongoni mwa watu, na sheria ambayo watu binafsi wanaishi kwayo katika maisha yao ya kila siku. Hili hupatikana kupitia taasisi na nidhamu zake zinazo kuza, kutabikisha, kupigia debe, kutekeleza na kulinda maadili na sheria za familia ya Kiislamu ndani ya mujtama.

(1) Khilafah ambayo imejengwa juu ya msingi safi wa Uislamu, itakuza TAQWA – uchamungu – ndani ya mujtama mzima kuliko kutafuta matakwa na matamanio ya kibinafsi yenye madhara kama yanavyo pigiwa debe kupitia uhuru ulio pitiliza na usawa wa kijinsia. Taqwa ndio msitari wa mbele wa ulinzi na kiungo muhimu zaidi cha kukuza na kulinda familia imara kwa sababu ndio msukumo mkuu wa matendo mema, kutimiza majukumu ya Mwenyezi Mungu (swt), na utiifu kwa Mipaka na Sheria Zake.

Taqwa humsukuma mtu binafsi kuingiliana na jinsi ya pili kwa Haya, kujifunga kwa sheria zote za kijamii katika makutano yao nao – ima iwe hadharani, faraghani au mtandaoni, kutafuta ndoa ili kuchunga shahwa, na kujiweka mbali kutokana na kitendo chochote au hali yoyote inayo karibia haramu ili kulinda heshima yao. Ni hili ndilo linalo punguza mahusiano nje ya ndoa katika mujtama. Ni Taqwa pia ndio inayomshajiisha mtu binafsi kutafuta mwenza kwa msingi wa Dini na tabia njema ili kuifanya ndoa kuwa fungamano la usuhuba. Na ni Taqwa ndio gundi inayo gandisha pamoja familia yenye mafanikio kwani humsukuma kila mwanafamilia kutekeleza majukumu yao na haki za wengine kwa uvumilivu, uangalifu na upole na kushirikiana juu ya wema na uchamungu, kuepuka uchoyo na ubinafsi na kutenda kile kilicho bora kwa maisha yao ya ndoa na familia. Hii hujumuisha kufanya kila kilicho muhimu ili kupata utulivu katika ndoa na kuepuka talaka. Hivyo, humshajiisha mwanamume kumtendea wema mkewe, kufanya bidii kutoa mahitaji ya familia yake na kutekeleza dori yake kama msimamizi kwa mapenzi, uangalifu, upole na huruma badala ya hofu na ghasia. Humshajiisha mwanamke kuwa mtiifu kwa mumewe, kutekeleza majukumu yake ya nyumbani kuzingatia uangalifu mkubwa, wakati na umakinifu katika kuwalea watoto wake. Na huwashajiisha watoto kuwaheshimu, kuwatii na kuwachunga wazazi wao na wakubwa zao … ikijenga maisha mazuri na familia yenye utulivu.

Khilafah hukuza Taqwa ndani ya mujtama kupitia utabikishaji wake kamili wa Uislamu. Nidhamu ya Elimu ya Khilafah kwa mfano itakuza maadili na ufahamu sahihi wa hukmu za kijamii na majukumu ya Kiislamu katika raia wake, kiasi ya kuwa mujtama kwa jumla utashikamana na sheria kupitia ukinaifu na mapenzi ya hukmu zake na kupinga tabia chafu na fisidifu kwa aina zake zote. Utekelezaji wa hukmu za Kiislamu kupitia nidhamu za kisiasa na mahakama za Khilafah zitaadhibu wale watakao kiuka mipaka ya Uislamu. Na Sera ya Vyombo vya Habari ya Khilafah itasaidia maslahi ya Uislamu, ikiwemo kupambana na fikra zozote fisidifu na kulingania kila kilicho kizuri. Magazeti, majarida, runinga, redio, mitandao ya kijamii, makongamano na mbinu nyenginezo zitatumiwa ili kufikia lengo hili.

(2) Khilafah itaupangilia mujtama juu ya msingi wa mtazamo sahihi wa mahusiano kati ya wanaume na wanawake unaoazimia ushirikiano baina ya jinsia hizo mbili huku pia ikilinda familia. Kupitia nidhamu yake ya elimu, vyombo vyake vya habari na utabikishaji wake kamilifu na utekelezaji wa maadili na hukmu za nidhamu ya kijamii ya Kiislamu, Khilafah itauelekeza mtazamo wa jamii juu ya uhusiano kati ya wanaume na wanawake kando na kupagawa na upande wa ngono na starehe kwa kile kilicho sambamba na lengo halisi la ghariza ya kijinsia na manufaa yake kwa mujtama – ndoa na kizazi. Hii ni kuongezea kupigia debe mtazamo wa wanawake kama heshima na umuhimu wa haya na kujistiri. Hivyo basi, itaharamisha kasumba mbovu ya kuwapa sura ya ngono wanawake na mujtama au kupigia debe mahusiano yoyote machafu ima katika unadi wa bidhaa, vyombo vya habari, fasihi au mtandaoni. Pamoja na hili, Khilafah itatabanni hijabu (khimar) na jilbab kama vazi la nje la mwanamke – awe Muislamu au asiyekuwa Muislamu – ikiharamisha kuonyesha uchi au mapambo katika maisha ya nje, ikisaidia kudumisha mahusiano safi baina ya wanaume na wanawake na kulinda sitara yao.

Dola pia itakomesha uchanganyikaji huru na faragha (khulwah) kwa wanaume na wanawake ulioko leo katika mashule, vyuo, vyuo vikuu, mabaa na vilabu, na sehemu nyinginezo na majumbani na ambao aghlabu hupelekea mahusiano nje ya ndoa, badala yake kutabikisha utenganishaji wa wanaume na wanawake sana iwezekanavyo katika maisha ya nje – ima katika taasisi zake za elimu, nidhamu yake ya usafiri, makazini, mahospitali na maeneo mengine.

“Kimsingi wanaume na wanawake hutenganishwa, na hawatangamani pamoja isipokuwa kwa ajili ya haja ambayo sheria imeiruhusu na imeruhusu kutangamana kwao ajili yake, kama vile biashara na hajj.”

Kifungu cha 113, Kielelezo cha Katiba ya Al-Khilafah cha Hizb ut Tahrir

“Hairuhusiwi kwa mwanamke kuwa peke yake na mtu asiyekuwa mahram yake. Hairuhusi kwake kuonyesha mapambo (Tabarruj) yake na uchi (‘Awrah) wake mbele ya wanaume wa kando.”

Kifungu cha 118, Kielelezo cha Katiba ya Al-Khilafah cha Hizb ut Tahrir

Pamoja na hili, Khilafah itashajiisha pakubwa na kusaidia ndoa, ikiwemo kifedha ikihitajika. Khalifah wa karne ya 8, Umar bin Abdul Aziz, kwa mfano, aliagiza mali ya dola kupewa wale waliohitaji kuoa. Fauka ya hayo, Uislamu umeweka adhabu kali ya zinaa inayo ashiria umakinifu ambao kwao Uislamu hutazama ulinzi wa ndoa na familia.

*Endelea Uk..16*

(3) Nidhamu za Khilafah zitasaidia utekelezaji wa dori za ndoa na familia za Kiislamu, na majukumu na haki za wanaume na wanawake ili kupatikane utulivu katika maisha ya ndoa na familia. Nidhamu yake ya elimu na vyombo vya habari zitajenga ufahamu safi wa hukmu za kisheria za Kiislamu ndani ya vijana na raia wake zinazo husiana na majukumu ya kibinafsi ya jinsia hizi mbili ndani ya maisha ya familia. Kwa mfano, katika masomo ya fiqh ya Kiislamu katika mtaala wake wa elimu, dola itakuza mtazamo sahihi wa majukumu na sifa za mwanamume kama msimamizi wa familia ambaye anapaswa kuwa na huruma, upole na uchungaji juu ya mkewe na watoto wake. Masomo haya pia yatajenga ufahamu wa umuhimu na majukumu ya wanawake katika dori yao msingi kama kina mama na wake pamoja na wachangiaji wakubwa wa maendeleo na ufanisi wa jamii na mujtama. Zaidi ya hayo, katika kiwango cha elimu ya shule ya upili, wanafunzi wa kike, mbali na kusoma masomo jumla kama vile thaqafa ya Kiislamu, hesabu na sayansi, watapewa vilevile chaguo la kuchukua Somo la Nyumbani litakalo wawezesha kupata taaluma katika nyanja za uangalizi na usimamizi wa watoto katika maisha ya nyumbani.

Khilafah haitaelimisha tu raia wake hukmu zinazo husiana na maisha ya familia pekee, bali itawasaidia kivitendo katika kutekeleza dori na majukumu yao. Kwa mfano, Kifungu cha 153, cha Kielelezo cha Katiba cha dola ya Al-Khilafah cha Hizb ut Tahrir, “Dola itadhamini kazi kwa raia wake wote wanaobeba uraia wa Dola.”

Jukumu hili juu ya Khilafah limejengwa juu ya Hadith ya Mtume (saw), «وَالإِمَامُ رَاعٍ وَمَسْئُولٌ عَنْ رَعِيَّتِهِ» “Imamu (Khalifah) ni mchungaji na ataulizwa kuhusu raia wake.” Hivyo basi, Khilafah itamsaidia kila mwanamume kutekeleza jukumu lake la kukimu mahitaji ya familia yake, ikiwemo kupeana pesa kutoka katika hazina yake, kupeana ardhi yake ya ukulima, na kuandaa mafunzo kwa wale wanao yahitaji kwa ajili ya ajira, na kuwawezesha kukimu maisha. Yote haya hupatikana kutokana na umbile sahihi la nidhamu ya kiuchumi ya Kiislamu inayo zalisha uchumi fanisi.

Vilevile, Khilafah itawawezesha wanawake kutekeleza dori yao msingi kama kina mama kupitia kuhakikisha kuwa daima wanaangaliwa kifedha na kamwe hawalazimishwi kulegeza msimamo kwa majukumu yao msingi kwa watoto wao kutokana na shinikizo la kiuchumi ili kupata ajira. Hivyo basi, mahakama za Khilafah zitamsaidia mwanamke yeyote ambaye mumewe amekataa kumkimu na watoto wake, na kumlazimisha kutekeleza jukumu lake hili kwa mujibu wa uwezo wake au kukabiliwa na adhabu endapo atakataa. Maandishi kutoka katika vitabu vya sheria vya wanazuoni wa Kiislamu wakati wa Khilafah ya Abbasiya, kwa mfano, yanaeleza namna gani wanawake walikuwa wakipeleka malalamishi yao kwa makadhi dhidi ya waume waliokuwa hawawakimu kwa masrufu ya kutosha na namna makadhi hao walivyo lazimisha malipo. Katika hali ambayo mume wa mwanamke ni masikini au hana ndugu wa kiume wa kumkimu, basi ni jukumu la Khilafah kufanya hivyo, kwani Mtume (saw) amesema «مَنْ تَرَكَ مَالاً فَلِأَهْلِهِ وَمَنْ تَرَكَ دَيْنًا أَوْ ضَيَاعًا فَإِلَيَّ وَعَلَيَّ» (رواه مسلم) “Yeyote anaye acha mali ni ya jamaa zake, na yeyote anaye acha deni au wanao mtegemea ni kwangu mimi na juu yangu.” Yote haya pia yatahakikisha kuwa watu binafsi hawatashinikizwa kupanga familia zao kwa kuhofia ufukara. Bali, Khilafah itashajiisha familia kuwa na watoto wengi kwa kutambua kuwa daima watapewa mahitaji yao.

“Moja wapo ya sifa nyingine nzuri ya tabia ya Waturuki ni ukarimu na heshima yao kwa Muumba wao … mama ni mshauri; hutafutwa ushauri wake, husitiriwa, husikizwa kwa heshima na utiifu, hukirimiwa hadi mwisho wake na kukumbukwa kwa mapenzi na majonzi kaburini mwake.”

Julie Pardoe, Mwanahistoria na Msafiri wa Kiingereza wa karne ya 19, akizungumzia kuhusu hadhi ya mama chini ya Khilafah Uthmaniya katika kitabu chake ‘Mji wa Sultan na Mienendo ya Kijamii ya Waturuki mnamo 1836’

Pamoja na yote haya, nidhamu ya kimahakama ya Khilafah itacheza dori muhimu katika kudumisha umoja na utulivu wa maisha ya ndoa na familia. Kamwe haitavumilia ghasia za kinyumbani, na kuwaadhibu vikali wahalifu wake. Itasimama kama mlinzi dhidi ya ndoa za lazima na kukabiliana vikali na vitendo vyovyote na mitazamo yoyote mengine ya kitamaduni isiyo kuwa ya Kiislamu inayo dhuru familia. Na itahudumu kama mwamuzi muhimu katika kutatua barabara na kwa haraka mizozo ya kindoa na familia ili kuzuia kukua kwa matatizo – kupitia kuhakikisha ufikiaji haki ni wa haraka, adilifu na huru.

• Hivyo basi, Khilafah itahudumu kama ngome halisi ya familia, ikiimarisha na kuilinda kutoka pembe zote. Hii ndio sababu mwanachuoni maarufu Imam Ghazali (RM) alisema, “Dini ndio msingi na Sultan ndiye mlinzi. Kitu kisicho kuwa na msingi huporomoka na kitu kisicho kuwa na mlinzi hupotea.”

ثُمَّ جَعَلْنَاكَ عَلَى شَرِيعَةٍ مِّنَ الْأَمْرِ فَاتَّبِعْهَا وَلَا تَتَّبِعْ أَهْوَاءَ الَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ

“Kisha tukakuweka wewe juu ya Sheria ya mambo yao, basi ifuate, wala usifuate matamanio ya wasio jua kitu.” [Al-Jathiya: 18]

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Dkt. Nazreen Nawaz**
**Mkurugenzi wa Kitengo cha Wanawake katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**